

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA TISA

29 APRILI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA TISA – TAREHE 29 APRILI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

218. MHESHIMIWA AISHA MSANTU MDUYAH (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawekea Miundombinu wezeshi Wanafunzi wenye mahitaji maalum ili wasome fani wanazozipenda.

219. MHESHIMIWA MARTHA NEHEMIA GWAU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaweka Sheria ya Ugatuzi wa Madaraka kwa Serikali za Mitaa kama hatua ya kutekeleza Dira ya Taifa ya 2050.

220. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (CHAMAZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Charambe Magengeni hadi Zahanati ya Kilamba ili kuondoa kero kwa Wagonjwa wanaoenda Hospitali ya Wilaya.

221. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Daraja linalounganisha Vijiji vya Wigelekelo Gumali, Masela na Barabara Kuu ya Mwigumbi Maswa.

222. MHESHIMIWA CHARLES JACOB SUNGURA (HANDENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Kwedikwazu - Sindenini inayopitia Daraja la Komdudu ambayo ipo kwenye Mradi wa *World Bank* kwa kiwango cha Lami.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

223. MHESHIMIWA DKT. NEEMA PETER MAJULE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali imeweka vivutio gani vya uwekezaji kwa Wazawa ili kuwahamasisha kuwekeza zaidi nchini.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

224. MHESHIMIWA DKT. CATHERINE CANUTE JOACHIM (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali imepata matokeo gani katika kupunguza uchafuzi wa mazingira tangu kuanza kwa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki mwaka 2019.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

225. MHESHIMIWA AMINA MUSSA MKUMBA (KIBITI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha VETA katika Jimbo la Kibiti.

WIZARA YA MAJI:

226. MHESHIMIWA ALAN THOMAS MVANO (KAKONKO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mkandarasi atakamilisha kuchimba na kujenga kisima cha maji katika Kijiji cha Kihomoka kama ilivyo kwenye Mkataba wake.

227. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji katika Kijiji cha Mpandapanda Kata ya Kiwira utaanza kutekelezwa.

228. MHESHIMIWA MARIRTA GIDO KIVUNGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali inampango gani wa kukamilisha ujenzi wa Miradi ya Maji iliyosimama kwenye Halmashauri za Wilaya ya Meru, Longido na Monduli.

WIZARA YA UCHUKUZI:

229. MHESHIMIWA JASMINE CHESCO NG'UMBI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali inampango gani wa kuwapatia Mafunzo ya kitaalamu Wahitimu wapya katika Sekta ya Uchukuzi ili kuongeza ajira.

WIZARA YA KILIMO:

230. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Mashamba yaliyokuwa ya Ngano nchini ili kuweza kukidhi mahitaji ya Ngano nchini.

WIZARA YA UJENZI:

231. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Mlowo - Kamsamba itaanza kujengwa kwa kuwa ni zaidi ya mwaka tangu Mkandarasi asaini Mkataba.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

232. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIM HALAMGA (HANANG’):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itaanzisha Kiwanda cha kuchakata Mazao katika Jimbo la Hanang’.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA KILIMO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
29 APRILI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**